

# Ninataka kupiga kura!

## Ninahitaji nini kupiga kura?

- **M** – kwa **-MAKAZI-** uthibitisho wa makazi utakapopigia kura : Leseni ya gari, kitambulisho cha wasioendesha magari, pasipoti, mkataba wa kupanga nyumba, bili ya umeme, maji, simu, inayoonyesha majina na anwani yako
- **K**- kwa **-KITAMBULISHO-**uthibitisho kuwa ni wewe ndiye mwenye kuhusika kwenye: Leseni ya gari, kitambulisho cha wasiondesha magari, pasipoti amabayo haijaisha muda, cheti cha kuzaliwa
- **U- URAIA-**Uthibitisho wa uraia wa Marekani: Cheti cha uraia (naturalization), pasipoti amabayo haijaisha muda, cheti cha kuzaliwa
- **U**- kwa **-UMRI-** uthibitisho kwamba utakuwa umefikisha miaka 18 siku ya kupiga kura, Leseni ya gari, kitambulisho cha wasioendesha magari, pasipoti, Cheti cha kuzaliwa

## Lini wapi nijiandikishe kupiga kura?

- Jumatatu – Ijumaa : saa mbili- saa kumi na moja jioni (8.00 am-5.00pm) City Hall, One City Hall Plaza katika barabara ya Elm Street
- Siku ya kupiga kura, kwenye kituo chako cha kupiga kura

## Itakuaje kama sina makaratasi ya uthibitisho nitakapokwenda kujiandikisha?

- Unaweza kutia sahihi kwenye hati ya kiapo ukidhibitisha kuwa una sifa zote zinazohitajika
- Baada ya kupiga kura maafisa wa City Hall watahakiki maelezo uliyoanadika kwenye fomu ya kiapo

## Ni wapi kilipo kituo changu cha kupigia kura? Niwapi nitapiga kura?

- Kwenye mtandao, katika tovuti ya City, [www.manchesternh.gov/election](http://www.manchesternh.gov/election)
- Bofya (bonyeza) kwenye, where do I vote? ingiza anwani yako

## Itakuwaje kama sitaweza kwenda kwenye kituo changu cha kupiga kura siku ile ya kupiga kura?

- Nenda City Hall mapema na kujiandikisha kupiga kura ya absentee ballot (kura inayopigwa mapema kwa sababu ya kutokuwepo siku ya kupiga kura)
- Ikiwa tayari umejiandikisha kupiga kura, unaweza kuprinti fomu ya maombi ya absentee ballot katika tovuti ya City, [www.manchesternh.gov](http://www.manchesternh.gov). (Bofya/bonyeza kwenye City Clerk, alafu kwenye elections)

Una Maswali? Wasiliana na ofisi ya City Clerk kwenye [cityclerk@manchesternh.gov](mailto:cityclerk@manchesternh.gov) au 603-624-6455

Imetayalishwa na Welcoming Manchester, email [welcomingmanchester@gmail.com](mailto:welcomingmanchester@gmail.com). Wasiliana nasi katika facebook na Manchester Community Action Coalition; email [grace@mcacnh.org](mailto:grace@mcacnh.org).

